# Misitu rasilimali inayonufaisha wananchi - Mjaja

**NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM**

IMEELEZWA kuwa hifadhi ya misitu ina tija na huwanufaisha wananchi wanaoishi kuzunguka maeneo ya hifadhi za misitu na kuokoa uchumi wa Zanzibar.

Mkuu wa wilaya ya Micheweni, Khatib Juma Mjaja, alieleza hayo katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani, wilaya ya Kusini Unguja wakati wa majumuisho ya ziara ya mafunzo iliyohusisha watendaji kutoka Pemba na Unguja kwa lengo la kubadilishana uzoefu baina ya hifadhi hiyo, hifadhi ya Ghuba ya Chwaka na hifadhi ya msitu wa kimaumbile Ngezi Vumawimbi.

Aidha Mjaja alisema misitu ni rasilimali inayokabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ya mabadiliko ya tabia ya nchi hivyo ni umuhimu kuhifadhiwa ili kukabiliana na athari za mabadiliko hayo.

Alieleza kuwa ujio wa ziara hiyo imewawezesha kuona vivutio mbali mbali vilivyomo katika msitu wa Jozani na kuona jinsi ya jamii inayoishi kando ya msitu huo wanavyoendelea kuuhifadhi na kunufaika nao kupitia jumuiya zilizopo katika maeneo yao.

Hivyo alisema kwa kuliona hilo na wao watahakikisha wanaenda kuyafanyia kazi mafunzo waliyoyapata ili na wanajamii wanaiozunguka misitu ya Ngezi waweze kunufaika.

"Msitu una rasilimali ya kujipatia kipato hivyo kukiwa na mgawanyo mzuri wa mapato yanayotokana na hifadhi, hamasa ya Jamii itaongezeka kwani yatasaidia kwenye jamii pamoja na serikali yenyewe", alieleza Mjaja.

Naye Afisa Mdhamini, Mhandisi Idriss Hassan Abdulla, alisema Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Serikali ya mkoa Kaskazini Pemba na Wilaya ya Micheweni watatekeleza hatua kwa hatua mmbo waliyoyaona katika ziara hiyo ili kuisaidia jamii inayozunguka hifadhi za misitu iliyopo huko.

"Tumekuja kujifunza na tumeona vivutio vingi hivyo na sisi tunakwenda kuhifadhi msitu wetu wa Ngezi Vumawimbi kuwa hifadhi nzuri uangalizi mzuri sambamba na kuitunza na kuongeza kipato cha Wananchi waliozunguka msitu huo" Alisema Idriss.

Naye Afisa Mkuu wa Misitu kutoka Idara ya Misitu Pemba, Samira Makame Juma, alieleza kuwa wamekua wakiwahamasisha wananchi kuendeleza miradi ya uhifadhi katika maeneo ya hifadhi pamoja na kuwapa elimu ili waweze kupata mafanikio.

Aliongeza kuwa ziara hiyo muhimu iliyowashirikisha Masheha ililenga kujenga hamasa na uelewa wa shughuli za kujiongezea kipati zinazoweza kufanyika katika hifadhi za misitu bila ya kuathiri ikolojia na mandhari ya misitu.

"Tumekuja kuona vivutio katika msitu wa Jozani pamoja na miradi inayotekelezwa na jamii wa maeneo hayo ili na wao waweze kupata fursa za kuweza kuibua miradi ambayo itaenda kuwaongezea kipato", alieleza.

Nao Masheha wa shehia zinazozunguka msitu wa Ngezi walisema kufuatia mafunzo waliyoyapata watawafundisha na wananchi wao njia bora za uhifadhi misitu kwa kuanziasha miradi ya kiuchumi.



*WANANCHI wa shehia za Mpendae kwa Binti Amran, Migombani na Kilimani wakipatiwa elimu ya sheria juu ya masuala mbali ya kijamii, wakati wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayoendelea kutolewa katika maeneo ya mkoa wa Mjini Magharibi. (NA MPIGA PICHA WETU).*

# 'Vyama vya ushirika chachu ya mabadiliko ya kilimo nchini'

**NA MWANDISHI WETU**

KATIKA kuunga mkono juhudi za kuinua sekta ya kilimo nchini, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imefanya mafunzo mahsusi kwa vyama vya ushirika mkoani Manyara kwa lengo la kubadilisha kilimo kuwa cha kibiashara na kuongeza kipato cha wakulima wa mazao ya mboga na bustani.

Afisa Ushirika Mwandamizi wa TCDC, Happiness Olotu, alisema hayo wakati akifunga mafunzo kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Mazao ya Bustani ikiwa ni utekelezaji wa mradi kwa awamu ya pili mwaka 2024/2025.

Aidha Olotu alisema kuwa mafunzo hayo yamefanyika katika wilaya ya Simanjiro, chama cha AMCOS Mirerani kilichopo Mererani, na wilaya ya Mbulu, vyama vya msingi Gidesha AMCOS na Sayuni Haydom SACCOS Ltd vinavyoshughulika na mazao ya mbogamboga.

Alisema mafunzo hayo yamegusa masuala ya uzalishaji wa kisasa, uongezaji thamani wa mazao, matumizi bora ya rasilimali ardhi pamoja na uelewa wa masoko, hatua inayolenga kuimarisha uwezo wa wakulima kuingia kwenye ushindani wa soko la kitaifa na kimataifa.

"Tunataka kuona vyama vya ushirika vikigeuka kuwa daraja la maendeleo kwa wakulima, si tu kwa uzalishaji bora, bali pia kwa kuwaunganisha na wadau wa masoko na mitaji", alisema Olotu.

Aliongeza kuwa ushirikiano kati ya Maafisa Ushirika na Maafisa Ugani katika maeneo husika ni muhimu kwa kuhakikisha wakulima wanafuatiliwa, wanashauriwa na wanasaidiwa katika hatua zote za utekelezaji wa maarifa waliyopewa.

Hivyo aliwataka wanachama wa vyama vilivyonufaika kutambua nafasi yao katika kuleta mabadiliko, wakitumia ujuzi walioupata kubadilisha maisha yao na jamii zao, huku akiwahakikishia usaidizi kutoka tume iwapo watakutana na changamoto.

Kwa mujibu wa Tume, jitihada hizi ni sehemu ya mkakati mpana wa kitaifa wa kuimarisha mfumo wa ushirika nchini, kwa kulifanya kuwa chombo imara cha kuinua wakulima wadogo kiuchumi na kuchochea maendeleo endelevu ya vijijini.

Kwa upande wake Afisa Kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Bahati Majaliwa, alisema Wizara inaendelea kuimarisha sekta ya ushirika kwa kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara wanachama wa vyama vya ushirika nchini ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea kiuchumi kupitia uzalishaji wa mazao kwa tija na kwa kuzingatia mahitaji ya soko.

# Ubora wa huduma waongeza mama wajawazito wanaojifungua hospitali

**NA MARYAM HASSAN**

IMEELEZWA kuwa kuimarika kwa miundombinu ya utoaji huduma za afya nchini na kuimarika kwa huduma zinazotolewa zimeongeza idadi ya mama wajawazito kujifungulia hospitalini.

Hali hiyo imethibitishwa na idadi ya mama wajawazito wanaofika katika hospitali za wilaya, mkoa na vituo vya afya vinavyotoa huduma za mama na mtoto na kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya mama na watoto wachanga wakiwemo wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti).

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi Daktari Dhamana wa hospitali ya wilaya kivunge, Dk. Haji Machano Haji, alisema uwepo wa miundombinu, vifaa tiba na dawa umechangia kuimarisha ufanisi wa kazi zao ikiwa ni pamoja na kushawishi wananchi kutumia hospitali kupata huduma

Akitolea mfano katika mkesha wa kuamkia sikukuu ya Eid el Hajj hospitalini hapo jumla ya watoto 11 walizaliwa, wakiwemo wanane waliozaliwa kwa njia ya kawaida na watatu kwa upasuaji kutokana na sababu mbali mbali ambapo kati yao sita walikuwa wanawake na watano wanaume.

"Tumekuwa tukipokea mama wajawazito wengi ambao kutokana na uwepo wa vifaa na watendaji wenye weledi tunaweza kuwahudumia na wengi wao wanatoka salama na wale wanaokuwa na mapingamizi yeyote tunawasaidia kwa kuwa uwezo huo tunao", alieleza Dk. Haji.

Naye Daktari Dhamana Hospitali ya Wilaya ya Chumbuni, Dk. Anthony Batlazary Ngowi, alisema kuwa katika kipindi hicho, watoto wanane walizaliwa kwa njia ya kawaida wakiwemo wanawake sita na watatu wanaume.

"Katika idadi hii mtoto mmoja alizaliwa kwa njia ya upasuaji lakini kwa bahati mbaya alifariki dunia", alieleza Dk. Ngowi na kuhimiza wananchi kutumia hospitali na vituo vya afya wakati wanapokuwa na changamoto za kiafya.

Aidha Daktari Dhamana katika Hospitali ya Mbuzini, Juma Khator Khamis, alisema kuwa wazazi saba walijifungua katika mkesha huo akiwemo mmoja aliyejifungua mapacha ambapo kati ya watoto wanane waliozaliwa, wanne ni wanawake na wanne wanaume.

Kwa upande wa Hospitali ya Rufaa Mnazimmoja, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha uhusiano hospitalini hapo, Ali Azizi Masoud, alieleza kuwa watoto sita walizaliwa ambapo watatu walikuwa wanawake na watatu wanaume huku Hospitali ya Mwembeladu, watoto watano wawa kiume wakizaliwa.

Kwa upande wa Hospitali ya Kitogani, Bakari Mohammed Faki, alisema kuwa watoto tisa (wanawake wanne na wanaume watano) walizaliwa wakati Katibu wa hospitali Wilaya ya Ijitmai, Seif Yahya Issa, akisema watoto wanane walizaliwa (wanawake sita na wanaume wawili) ambapo haya hivyo mtoto mmoja alifariki dunia lakini hali ya mama wa mtoto huyo inaendelea vizuri.

Kutoka na taarifa za madaktari hao, jumla ya watoto 55 (wanawake 29 wanaume 26) walizaliwa katika mkesha wa sikukuu hiyo katika hospitali za Unguja pekee hali inayoashiria kuongezeka kwa watu wanaotumia huduma za afya zikiwemo za mama na watoto.